
# NINYI NYOTE TUNAWASALIMIA

(NO.2)

Mtunzi: IRA. M. Jules
Date: 19/ 06/ 2022
Choir: St. Anna Maria




## SOMA MANENO

Mabet:

1. Tunawasalimia wakristo wa hapa kigongo cha Familia takatifu,
   Tunawasalimia wakristo kutoka kigango cha Roho Mtakatifu,
   Wengine tuliokuja nao kutoka kigango cha Mtaktifu Paulo Mtume
   na wengine kutoka sehemu mbalimbali tunawasalimia. + ***Kiitikio.***

2. Hizi ni neema za Mungu ametujalia leo ili tukae pamoja kwa siku hii
   ya leo ee jamaa mlio kuwa hapa njoni tumsifu Mungu wetu milele yote. + ***Kiitikio.***

3. Hizi ni neema tumepewa na Mungu katuamsha salama hakuna chochote
   tumetoa kwake, tumekuja hapa na tukafika salama na ndio maana sisi
   KWAYA YA MTAKATIFU ANNA MARIA tunawasalimia tukisema. + ***Kitikio.***

4. Siku hii ya leo Mwenyezi Mungu ametujalia uhai, kuna wengine wameshaaga
   dunia hii, na wengine wamelazwa hospitalini nasi kwa uhai na kujivunia upendo
   wa Mungu kwetu ndio maana tunawasalimia tukisema. + ***Kiitikio.***

***N. B:*** *1. Muimbaji akiwa anasoma meneno ya mabet Organist anaendelea kucheza Free Organ ambao inaendana na jinsi msomaji wa mabet anavyosoma.*
*2. Kutokana na sehemu ulipo unaweza kubadilisha maneno fulani ya mabet.*

67899059 - 0758272224
Copied by: JIRAM